

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI
MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

636

TEHAMA

Muda: Saa 3

Alhamisi, 08 Mei 2014 mchana

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A na B.
2. Jibu maswali yote katika sehemu A na maswali **manne (4)** kutoka sehemu B.
3. Zingatia maelekezo ya kila sehemu na ya kila swali.
4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.



SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Bainisha kwa kifupi misingi minne ya ufundishaji wa somo la TEHAMA.
2. Onesha matumizi ya vipengele vinne muhimu vinavyounda muhtasari wa somo la TEHAMA.
3. Toa sababu nne zinazoweza kumfanya mwalimu wa somo la TEHAMA kufaragua zana za kufundishia somo hilo.
4. Eleza kwa kifupi namna mwalimu wa somo la TEHAMA anavyoweza kutumia mada iliyoandikwa gazetini kufundishia mada ya usikivu.
5. Onesha dhima nne za kufundisha mada ya alama za kuashiria hatari kwa wanafunzi wa shule za msingi.
6. Pendekeza mbinu nne zinazoweza kutumika kufundishia mada ya kueleza kwa ufasaha habari iliyosemwa kwa wanafunzi wa darasa la kwanza.
7. Bainisha mambo muhimu manne ya kuzingatia katika utunzi wa mitihani.
8. Eleza dhana zifuatazo kama zinavyotumika katika somo la TEHAMA.
(a) Upimaji (c) Upimaji tamati
(b) Tathmini (d) Upimaji endelezi.
9. Kwa kutoa mifano, eleza kwa kifupi faida nne za matumizi ya huduma za posta katika jamii.
10. Bainisha mambo manne unayotakiwa kuzingatia wakati wa kutumia maktaba.

SEHEMU B (Alama 60)

Jibu maswali **manne (4)** kutoka sehemu hii.

11. Kwa kutumia mifano, chambua faida tatu na hasara mbili za matumizi ya mitandao ya kijamii katika Intaneti.
12. Tathmini umuhimu wa mawasiliano ya kisasa katika kuendeleza taaluma na kukuza ufahamu wa wanafunzi katika ufundishaji na ujifunzaji (Toa hoja tano).
13. Kwa kutumia hoja tano, fafania umuhimu wa mwalimu kuzijaribu zana za kufundishia kabla ya kuzitumia darasani.
14. Eleza umuhimu wa vyombo vya mawasiliano ya kisasa katika kukuza maendeleo ya nchi kiuchumi, kisiasa na kijamii.
15. Fafania mambo matano yanayoweza kumtokea binadamu na kusababisha kuhitaji msaada wa ushauri nasaha.

16. Eleza kanuni tano za kuzingatia wakati wa kutunga jaribio au mtihani unaohusisha maswali ya kuoanisha katika somo la TEHAMA.
17. Fafanua faida tano za kufaragua na kutengeneza zana za kufundishia na kujifunzia somo la TEHAMA.
18. Eleza mambo matano yanayobainisha umuhimu wa matumizi ya Kompyuta kama chombo cha mawasiliano katika jamii.